**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA – MPANDA**



# MKUTANO MAALUM WA BARAZA LA MADIWANI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 UTAKAOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA YA MPANDA TAREHE 25/07/2018 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI

**Imetayarishwa na**:


OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA,

HALMASHAURI YA MANISPAA,

S.L.P. 216,

MPANDA

SIMU NA 025-252957128,

FAX NA 025-252957129

Email: md@mpandamc.go.tz


**JULAI, 2018**

**AGENDA ZA MKUTANO MAALUM WA BARAZA LA MADIWANI KUJADILI HOJA ZA MKAGUZI WA NJE KWA KIPINDI KINACHOISHIA JUNI 30.06.2017**

1) KUFUNGUA MKUTANO

2) KURIDHIA AGENDA ZA MKUTANO

3) KUJADILI UTEKELEZAJI WA MAJIBU YA MENEJIMENTI YA HOJA ZA MKAGUZI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30.06.2017

4) MAAGIZO NA MAELEKEZO YA MHESHIMIWA MKUU WA MKOA

5) KUFUNGA KIKAO

## MUHTASARI WA HOJA ZA UKAGUZI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2013-2017 ZILIZOJITOKEZA KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA

| MWAKA | HOJA ZILIZOJITOKEZA | JUMLA YA HOJA ZILIZOJIBUWA KIKAMILIFU NA KUFUNGWA | ASILIMIA | JUMLA YA HOJA AMBAZO HAZIJAPATIWA MAJIBU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 2013/2014 | 44 | 41 | 93 | 3 | 7 |
| 2014/2015 | 48 | 39 | 81 | 9 | 19 |
| 2015/2016 | 48 | 38 | 79 | 10 | 21 |
| 2016/2017 | 58 | 31 | 54 | 27 | 47 |
| JUMLA | 198 | 149 | 75 | 49 | 25 |

**UTEKELEZAJI WA MAJIBU YA HOJA ZA UKAGUZI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30.06.2017**

| MWAKA WA HOJA | AYA.NA | HOJA YA UKAGUZI | USHAURI WA MKAGUZI | UTEKELEZAJI WA MAJIBU YA HOJA | MAONI YA MKAGUZI | MAONI YA KAMATI YA FEDHA | MAONI YA BARAZA LA MADIWANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2016/17** | **2.1.1** | **Zidio la TZS 698,197,194 katika Makusanyo ya Ndani.** Mwaka 2016/2017 Halmashauri ilikisia kukusanya jumla ya Tsh. 2,023,510,000 kutoka makusanyo yake ya ndani na ilifanikiwa kukusanya jumla ya Tsh. 2,721,707,194 na kufanya zidio la makusanyo la Tsh. 698,197,194 sawa na aslimia 34.5. | Halmashauri inashauriwa kuongeza jitihada katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuhakikisha inapanga bajeti yenye uhalisia. | Mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ilikisia kukusanya Tsh. 2,023,510,000 kutoka makusanyo ya ndani na ilifanikiwa kukusanya Tsh.2,721,707,194 ikiwa na zidio la TZS 698,197,194 sawa na asilimia 34.5. Mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imeandaa bajeti yenye uhalisia na mikakati mbalimbali kuhakikisha makusanyo ya ndani yanaongezeka sambamba na udhibiti wa ndani wa mapato kama ifuatavyo:-<br>-Halmashauri ilikubali kupunguza mawakala wa ukusanyaji mapato na kukusanya yenyewe kwa kutumia watumishi wake.<br>-Kwa msaada wa mradi wa uboreshaji miji (ULGSP) Halmashauri ilipata mfumo wa kukusanyia mapato (LGRCIS).<br>-Kuanzisha matumizi ya | **Mkaguzi ameridhia Utekelezaji wa Menejimenti Hoja imefungwa** | Hoja kama hii isijirudie tena. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mfumo wa kukusanya mapato kwa njia ya mashine za kielekroniki (POS),<br>-Kuanzisha chanzo kipya cha mapato cha ushuru wa maegesho. Mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ilikisia kukusanya TZS 2,378,800,000.00 kutoka makusanyo ya ndani na ilifanikiwa kukusanya TZS1,581,945,937.94 hadi Machi 2018 ikiwa ni sawa na asilimia 66.5 ya Mwaka. | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2.2.1** | **Uwepo wa wadaiwa sugu TZS 638,760,002** | • Halmashauri inashauriwa kuandaa mkakati mahususi wa kufualia madeni.<br>• Umri wa madeni yaandaliwe na yawasilishwe kwa uhakiki. | Halmashauri ilikuwa inadai madeni yenye thamani ya Tsh 638,760,002.00 toka serikali kuu. Hazina wamepunguza deni la Tsh117,388,220.00 tarehe28/02.2018. na kubakiwa na deni la Tsh521,371,782.00 ambalo ni 30% ya kodi ya Ardhi Tsh129,141,098.00 toka Wizara ya Ardhi Nyumba na Makazi Tsh 392,230,684.00 madeni ya watumishi yasiyo ya mishahara ambayo yaliwasilishwa Hazina na fedha bado hazijapokelewa kutoka Hazina. | **Halmashauri inasisitizwa kuendelea kufuatilia madeni hayo.** | Halmashauri iendelee kufuatilia iliserikali ilipe madeni hayo. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2.2 | **Uwepo wa madeni ya muda mrefu TZS 1,897,990,105.** | • Halmashauri inashauriwa kuwa na mkakati madhubuti wa kukusanya mapato ya serikali.<br>• Umri wa madeni yaandaliwe na yawasilishwe kwa uhakiki. | Halmashauri imelipa madeni la TZS 1,321,351,931.25 bado TZS 576,638,173.75 na nyaraka zimewasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.<br><br>Madeni yote ni ya mwaka 2016/2017. | **Halmashauri inasisitizwa kuendelea kulipa madeni yaliyosalia.** | Halmashauri iendelee kufuatilia ili serikali ilipe madeni hayo. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2.3 | **Kushindwa kuwasilishwa kwa Kitabu cha mali za kudumu za Halmashauri.** | Menejimenti inatakiwa kuhakikisha kuwa kitabu cha mali za kudumu za Halmashauri kinaandaliwa kwa kuzingatia kikamilifu vipengele vyote kwa mujibu wa taratibu na kanuni na pia kuhakikisha uhuishwaji unafanywa pia kwa kuzingatia taraibu na vipenele vyote mathalani tarehe ya mapokezi, gharama, n.k. Aidha usuluhisho ufanywe kati ya Leja ya mali za kudumu na Taarifa kuu ya usuluhisho. | Kitabu cha mali za kudumu kiliandaliwa na kuwasilishwa kwa Mkaguzi kwa ajili ya uhakiki. Aidha menejimenti itahakikisha uhuishaji unafanywa kwa wakati. | **Mkaguzi ameridhia Utekelezaji wa Menejimenti Hoja imefungwa** | Hoja kama hii isijirudie tena. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2.4 | Kushindwa kutumia fedha za serikali TZS 4,147,870,355.00 | Menejimenti inatakiwa kuwasilisha mpango halisi wa matumizi ukionesha kiasi hicho kitakavyotumika kutekeleza miradi ambayo haijakamilika. | Taarifa ya utekelezaji wa miradi imeandaliwa kulinga na shughuli husika na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. | **Uhakiki wa utekelezaji wa majibu ya menejimenti utafanyika katika ukaguzi ujao.** | Halmashauri ilipe wazabuni kila wanapomaliza kazi. | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2.3.1** | **Kuwepo kwa kesi/mashauri matatu(3) katika Mahakama yenye gharama ya TZS 307,909,938**<br><br>Mapatio ya nyaraka mbalimbal yalibaini kuwa Halmashauri ina jumla ya mashauri matatu (3) katika mahakama yenye jumla ya gharama ya TZS 307,909,938 yakisubiri uamuzi wa mahakama husika. | Halmahauri kuptia kitengo cha Sheria ihakikishe kuwa mashauri haya yanasimamiwa vizuri kuepuka kushindwa kesi ambapo inaweza kusababisha hasara ya kifedha katika uendeshaji wa Halmashauri.<br>Aidha, tunaitaka Halmashauri izingatie utatuzi wa kesi nje ya Mahakama ili kupunguza gharama zinazoweza kujitokeza kutokana na fine, riba na ada za kisheria. | Mashuri baadhi yameamuliwa na Mahakama isipokuwa kesi ya moja ya MS O. Kalifumu. Halmashauri imeshinda katika mashauri hayo bado kesi moja.. | **Vielelezo vya Halmashauri kushinda kesi hizo vifuatiliwe na kuwasilishwa kwa mkaguzi, Pia Halmashauri ijitahidi kusimamia kesi iliyobaki.** | **Hati za hukumu ziletwe** | |
| | **2.4.1** | **Vyombo vya Moto Vilivyotelekezwa bila Kufanyiwa Matengenezo.**<br>Kanuni ya 45 ya MGFM inataka mali zote | Tunaitaka Menejimenti ihakikishe mali hizo zinauzwa. | Halmashauri imepokea kibali cha kuyauza magari kutoka Wizarani, mnada wa hadhara utafanyika tarehe 18/07/2018 baada ya | **Menejimenti ihakikishe mnadaunafanyika kwa tarehe iliyopangwa** | Halmashauri iwasilishe taarifa ya uuzaji wa vyombo vya moto tarehe | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | zisizotumika, zisizotengenezeka au 'skrepa' zibainishwe na kuuzwa au kuteketezwa baada ya kupata idhini kutoka kwenye Kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala.<br>Kinyume na matakwa na Kanuni iliyotajwa hapo juu, magari manne, pikipiki 13 na mitambo 2 imewekwa kwa maamuzi ya kuuzwa. | | taratibu zote kuwa zimekamilika. | | 18/07/2018 | |
| | **2.5.1** | **Manunuzi ya Bidhaa na Huduma Yaliyofanywa zaidi ya Ukomo wa Manunuzi bila Idhini ya Bodi ya Zabuni TZS 33,565,473.45**<br>Ukaguzi ulibaini kuwa katika mwaka 2016/2017, Halmashauri ilifanya malipo kwa wazabuni mbalimbali kwa ajili ya bidhaa na huduma zenye gharama ya TZS 33,565,473.45 kiasi hiki kinazidi ukomo wa kiwango cha TZS 3,000,000 ambacho Mkuu wa idara na Afisa Masuhuli anaruhusiwa kuidhinisha kwa kila mkataba kama inavyoelekezwa na kanuni ya 27(1) na Nyongeza ya Kwanza ya Mwongozo wa | Halmashauri inatakiwa izingatie taratibu za manunuzi ili kuepusha ununuzi wa bidhaa zisizo na ubora na bei zisizo elekezi. | Menejimenti itazingatia ushauri wa Mkaguzi. Manunuzi kwa baadaye yatafanyika kwa kufuata maelekezo ya Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za Manunuzi ya Umma. | **Menejimenti inashauriwa kuzingatia kanuni za manunuzi za mwaka 2013** | **Menejimenti inashauriwa kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi za mwaka 2013** | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Uundaji na Uendendeshaji wa Bodi ya Zabuni katika Serikali za Mitaa ya Mwaka 2007.<br>Aidha, hakuna idhini iliyotolewa na Katibu wa Bodi ya Zabuni kinyume na maelekezo ya kanuni ya 27(2) ya Mwongozo uliotajwa hapo juu. | | | | | |
| | **2.5.2** | **Kutokamilika kwa Makabidhiano ya Ununuzi wa pikipiki zenye Gharama ya TZS 6,549,400.00.**<br>Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ililipa TZS 6,549,400.00 kwa Shabir Hasanali kwa ajili ya ununuzi wa pikipiki kwa matumizi ya maafisa mapato katika Halmashauri. | Halmashauri inashauriwa kufuatilia na kuhakikisha kadi za pikipiki na namba za usajili zinapokelewa haraka iwezekanavyo.<br>Hata hivyo, mahojiano yaliyofanyika na Afisa Usafirishaji sambamba na mapitio ya nyaraka za manunuzi ilibainika kuwa :<br>Pikipiki zilipokelewa kupitia hati namba 0002239 na 0002240 zilizokabidhiwa kwa Afisa Mapato wa Manispaa, lakini kadi za pikipiki bado hazijawasilishwa na wazabuni.<br>Aidha ilibainika kuwa magari na pikipiki yalikuwa na namba binafsi badala ya namba za usajili za Serikali.<br>Hakuna ushahidi uliothibitisha kuwa pikipiki | Kadi za Pikipiki zote tatu zimewasilishwa na mzabuni zikiwa na namba MC943BGY, MC956BGY na MC187BGogre, usajili wa pikipiki hizo kwa namba za serikali unaendelea, baada ya kukamilika kadi zitawasilishwa kwa Mkaguzi kwa uhakiki.<br>Kwa kuongezea pikipiki zimeingizwa pia kwenye rejista ya mali za kudumu za Halmashauri. | **Mchakato wa usajili uendelee.** | **Atumwe mtu kufuatilia kadi za namba za serikali.** | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | hizo zilikaguliwa na zimekatiwa bima. | | | | |
| | **2.6.1** | **Kiasi ambacho Hakikulipwa kwenye Vijiji 60% ya Mapato ya Ndani TZS 1,178,193,521.82**<br>Halmashauri inatakiwa kuchangia 60% ya makuanyo yake ya ndani katika Miradi y Maendeleo ngazi ya Vijiji.<br>Mwaka 2016/2017 Halmashauri ilikusanya jumla ya TZS 2,721,707,194 kutoka makusanyo ya ndani ambapo kiasi cha TZS 1,633,024,316 kilitakiwa kipelekwe kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, Halmashauri iliilichangia TZS 454,830,794.58 tu sawa na aslimia 28 ya kiasi kilichokuwa kinatakiwa kuchangiwa na hivyo kubaki | Halamashauri inashauriwa kuongeza mchango kutoka katika makusanyo yake ya ndani kwenda kwenye miradi ya maendeleo. | Halmashauri ilichangia kiasi cha TZS 307,938,023.40 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na TZS 454,830,794.58 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwenda ngazi ya Kata, kijiji na Mitaa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 hadi Machi 2018 imechangia TZS 535,908,046.64 kulingana na uwezo wake wa mapato, mapato ya ndani yaliyobakia yametumika kuendesha shughuli za kila siku za Halmashauri | **Mkaguzi ameridhia Utekelezaji wa Menejimenti Hoja imefungwa** | Hoja kama hii isijirudie tena. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kiasi cha TZS 1,178,193,521.82 sawa na asilimia 72 ambacho hakikuchangiwa. | | | | | |
| | **2.6.2** | **Kutotolewa kwa Fidia ya Ruzuku Kutoka Wizara ya Fedha.**<br><br>Serikali kuu kupitia Wizara ya Fedha inatakiwa kufidia Halmashauri kwa vyanzo ambavyo vimefutwa.Kulingana na maelezo , 20% ya fidia hiyo inatakiwa ipelekwa katika ngazi ya Kata na Vijiji kusaidia maendeleo.<br>Mwaka wa fedha 2016/17 Serikali haikutoa fedha kwa ajili ya kufidia kodi ambazo zilifutwa na hivyo Halamshauri hazikuweza kupeleka katika ngazi za Kata na Vijiji 20% kama inavyotakiwa. | Menejimenti iwasiliane na Wizara ya Fedha ili kuona uwezekano wa kufidia kiasi ambacho hakijalipwa katika vijiji kwa mwaka 2016/2017. | Halmashauri imewasiliana na Sekretarieti ya Mkoa ili ufanyike mchakato wa kuwasiliana na Wizara ya Fedha kupitia barua Na. KTV/MTC/W.10/02 /135 ya tarehe 29th Mei 2017. | **Mkaguzi ameridhia Utekelezaji wa Menejimenti**<br>**Hoja imefungwa** | Hoja kama hii isijirudie tena. | |
| | **2.7.1** | **Upungufu wa Watumishi 412.**<br><br>Ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za kila siku unategemea uwepo wa rasilimali na rasilimali watu ya kutosha.<br>Mapitio ya ukaguzi yalibaini upungufu wa watumishi 412. | Tunasisitiza Menejimenti iwasiliane na Ofisi ya Rais katika Utumishi wa Umma kuajiri watumishi zaidi ili kuondoa upungufu uliopo. | Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, Halmashauri imekuwa ikipanga bajeti kwa ajili ya nafasi mbalimbali za ajira zilizowazi katika idara mbalimbali. Hata hivyo, changamoto inatokana na serikali kutotoa vibali vya ajira kama vinavyoombwa. Mathalani, mwaka | **Halmashauri inasisitizwa kuendelea kuomba kibali cha kuajiri ili kuondoa upungufu wa watumishi** | **Menejimenti iendelee kufuatilia kibali** | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 2015/2016 Halmashauri ilitenga bajeti ya ajira mpya 110, mwaka 2016/2017 Halmashauri ilitenga bajeti kwa ajili ya ajira mpya 62 na mwaka 2017/2018 Halmashauri ilitenga bajeti kwa ajili ya ajira mpya 352 na kufanya jumla ya ajira mpya kuwa 424 kama kibali kingetolewa kwa wakati.Vitabu vya bajeti vipo kwa ajili ya uthibitisho. | | | |
| | **2.7.2** | **Ajira Kutolewa kwa Watumishi 78 Wasiokuwa na Sifa na Kulipwa Mshahara.** Kifungu D.6(2) cha Kanuni za Utumishi wa Umma 2009) kinaelekeza kuwa, " Mtu hatateuliwa, kupandishwa cheo au kuhamishiwa katika nafasi yoyote katika utumishi wa Umma isipokuwa ana sifa zinazotakiwa kwa wakati huo." Ukaguzi katika taarifa za ukomo wa utumishi, majalada ya watumishi na mahojiano yaliyofanywa na Afisa Rasilimali watu ilibainika kuwa watumishi waliokuwa wameajiriwa na Halmashauri hawakuwa na sifa stahiki. Baada ya upelelezi watumishi husika | Kipindi kijacho Halmashauri izingatie maelekezo ya kifungu D.6 (1) na D.7 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2009. Halamshauri irejeshe mishahara yote iliyolipwa kwa watumishi wasio na sifa. | Watumishi waliotajwa walipatikana na makosa ya kugushi vyeti na wengine ni wastaafu. Watumishi hao waliondolewa kwenye mfumo wa malipo kwa wakati kati yao watatu (3) walikuwa na uhamisho wa muda na sio kutoroka na watumishi wanane (8) waliondolewa kwa sababu za kawaida kama kifo na kustaafu kisheria. | **Mkaguzi ameridhia Utekelezaji wa Menejimenti Hoja imefungwa** | Hoja kama hii isijirudie tena. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | walifukuzwa kazi na kutakiwa kurejesha fedha ya mishahara waliyokuwa wamelipwa. | | | | | |
| | **2.7.3** | **Watumishi Kukaimu katika Nafasi Zilizowazi.** Ukaguzi katika Idara ya Utumishi ulibaini kuwa Manispaa ya Mpanda ina upungufu wa watumishi wenye sifa za kujaza nafasi za juu katika idara/vitengo. Baadhi ya nafasi ama ziko wazi au zinakaimiwa na watumishi. | Tunashauri Halmashauri ichukue hatua kuhakikisha nafasi muhimu zinajazwa na watumishi wenye sifa ili Halmashauri iweze kutekeleza malengo yaliyokusudiwa. | Manispaa ya Mpanda imeanza kuchukua hatua kuhakikisha nafasi zilizo wazi zinajazwa na watumishi wenye sifa kwa kuandika barua za siri kwa Waziri mwenye dhamana ya upekuzi ili kupata wakuu kamili wa idara na vitengo. Mpaka sasa amethibitishwa Mkuu wa Idara ya Afya, Dkt. Obed Mahenge ambaye mchakato wake ulikamilika mwezi Oktoba, 2017,na nafasi ya Mwanasheria imejazwa.. | **Nafasi zilizobakia zijazwe na watumishi wenye sifa.** | Menejimenti iendelee kufuatilia vibali vya ajira. | |
| | **2.7.4** | **Watumishi ambao Hawajathibitishwa katika Mfumo wa HCMIS-Lawson** Ukaguzi katika hati za malipo kwa kuzingatia taarifa za hali ya uthibitisho wa watumishi ilibainika kuwa, baadhi ya watumishi walikuwa hawajathibitihwa japokuwa wamekuwa katika utumishi kwa zaidi ya miaka mitatu na | Maafisa Rasilimali watu wanashauriwa kuhakikisha uboreshaji wa data unafanyika ili kuwa na taarifa sahihi. | Maafisa Rasilimali watu wanaotumia mfumo wanaruhusiwa kufanya tu yale yanayoelekezwa katika PA 52.1, tofauti na hayo hawana uwezo wa kuingia kwenye mfumo. | **Mkaguzi ameridhia Utekelezaji wa Menejimenti Hoja imefungwa** | Hoja kama hii isijirudie tena. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | wengine tarifa za hali ya kuthibitishwa hazikuoneshwa. | | | | | |
| | **2.8.1** | **Ufanisi Mdogo wa Kamati ya Ukaguzi**<br>Waraka Na. 3/215/01 wa Mwezi Novemba, 2007 uliotolewa na OR-TAMISEMI unazitaka Halmashauri nchini kuunda Kamati ya Ukaguzi. Kamati hii inatakiwa kuangalia kwa kina mipango kazi ya ukaguzi wa nje na wa ndani kufanya tathmini ya mahitaji ya rasilimali za ukaguzi na kuweka uhusiano kati ya wakaguzi na Halmashauri. Kamati ya Ukaguzi inatakiwa kuhakikisha kuwa matokeo ya ukaguzi yanatolewa na mapendekezo na hatua zilizochukuliwa zinatekelezwa.<br><br>Katika mwaka wa ukaguzi, libainika kuwa Kamati ya Ukaguzi iliundwa lakini haifanyi kazi zake kwa ufanisi kama iavyoelekezwa kati Kanuni 12(1) ya Kanuni za Fedha2009.<br>Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-<br><br>Hakuna uthibitisho kwamba | Halmashauri ihakikishe kuwa Kamati ya Ukaguzi inafanya shughuli zake kwa ufanisi na kuhakikisha kuwa matokeo ya ukaguzi yanatolewa na mapendekezo na hatua zilizochukuliwa zinatekelezwa kikamilifu. | Kamati inatekeleza majukumu yake kikamilifu kama inavyoelekezwa katika 12(1) ya Kanuni za Fedha za mwaka 2009.<br>Mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ya Ukaguzi ilijadili hoja za Mkaguzi wa nje tarehe 14/09/2017 kabla ya kuwasilisha mapendekezo yake kwa menejimenti ya Halmashauri na Ofisi ya Mkaguzi Mkazi wa Hesabu wa Serikali. | **Menejimenti isubiri uhakiki huo.** | Menejimenti izingatie kuiboresha kamati hiyo. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Hoja za Mkaguzi wa Nje zilijadiliwa katika vikao vya Kamati ya Ukaguzi.<br>Jalada la Kamati ya Ukaguzi lilikaguliwa na kubainika kuwa hakuna uthibitisho kuwa Kamati ya Ukaguzi ilipitia kwa kina na kwa wakati mapendekezo na ushauri wa Mkaguzi wa nje. | | | | | |
| | **2.8.2** | **Kutojitosheleza kwa rasilimali watu katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani**<br>Kifungu cha 45 (1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya Mwaka 1982 (Iliyofanyiwa Marekebisho 2000) inamtaka Afisa Masuhuli kuunda Kitengo imara cha Ukaguzi wa ndani. Kanuni ya 14 ya LGFM, 2009 kinakitaka Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kusimamia matumizi. Hata hivyo, katika ukaguzi wa Kitengo cha Ukaguzi tulibaini ukosefu wa rasilimali fedha za kusaidia Kitengo Kuendesha shughuli zake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kutembelea maeneo ya miradi mikubwa ili kufanya tathmini ya maendeleo ya miradi husika. Hali hii inaweza kusababisha Kitengo kutofikia maeneo | Tunaishauri Halmashauri isaidie Kitengo cha Ukaguzi kifedha ili kiweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi. | Halmashauri hutenga bajeti ya ajira mpya kila mwaka kwa ajili ya kuongeza rasilimali watu. Mathalani, mwaka 2015/2016 Halmashauri ilitenga bajeti ya ajira mpya 110, mwaka 2016/2017 Halmashauri ilitenga bajeti kwa ajili ya ajira mpya 62 na mwaka 2017/2018 Halmashauri ilitenga bajeti kwa ajili ya ajira mpya 352 kati ya hizo 3 ni kwa ajili ya kitengo cha ukaguzi wa ndani na kufanya jumla ya ajira mpya kuwa 424 kama kibali kingetolewa kwa wakati. Vitabu vya bajeti vipo kwa ajili ya uthibitisho.<br><br>Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 bajeti ya Kitengo cha Ukaguzi kimeongezeka mpaka kufikia TZS 26,546,500 kwa mchanganuo ufuatao:- | **Utendaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani utahakikiwa katika ukaguzi ujao.** | **Kitengo kiwezeshwe kujengewa uwezo kibajeti na kiutumishi.** | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | mengi kiutendaji.<br>Pia tulibaini Kitengo kutokuwa na rasilimali watu ya kutosha. Kitengo hufanya ufuatiliaji wa miradi usimamizi wa rasilimali fedha lakini kina watumishi wawili tu. | | - TZS 17,550,000 mapato ya ndani na -TZS 8,996,500 Ruzuku kutoka Serikali kuu. | | | |
| | **2.8.3** | **Ufanisi Hafifu katika Udhibiti wa Mazingira ya Mfumo wa Teknolojia na Mawasiliano.**<br>Manispaa ya Mpanda inaendesha shughuli zake kwa njia ya mifumo ya Teknologia na Mawasiliano ambayo ni EPICOR, HRCMIS na LGRCIS.<br><br>Ukaguzi uliofanyika katika utendaji kazi wa mifumo hii ulibaini kasoro mbalimbali ikiwemo:- | Menejimenti inashauriwa kuchukua hatua za haraka kuboresha mazingira ya mfumo wa Teknolojia na Mawasiliano. | Halmashsuri inatarajia kuunda Kamati ya uendeshaji wa mfumo wa Teknolojia na Mawasiano katika mwaka wa fedha 2018/2019.<br>Kitengo cha TEHAMA kwa sasa kina watumishi 02 ambao husaidia uendeshaji wa mfumo wa Teknolojia na Mawasilano.<br>Kitengo kina Sera ya TEHAMA pamoja na Mpango Mkakati. | **Utendaji wa kitengo cha TEHAMA mchakato uendelee.** | Menejimenti iangalie kwa udharura kumpata Afisa Tehama. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | -Halmashauri kukosa Kamati ya Mkakati wa Teknolojia na Mawasiliano<br>-Halmashauri kukosa Kamati hai ya uendeshaji wa mfumo wa Teknolojia na Mawasiliano.<br>-Halmashauri kukosa mifumo ya udhibiti wa mazingira kama vile, mfumo wa kuzuia moto, vifaa vya kuzima moto, jenereta, viyoyozi(hasa katika vyumba vyenye komputa) na mfumo wa kudhibiti unyevu na joto.<br>-Hakuna mpango wa ahueni ya majanga. | | | | | |
| | **2.8.4** | **Mapungufu katika Tathimini ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani**<br>Ukaguzi kuhusu mfumo wa udhibiti wa ndani wa Halmashauri ulibaini mapungufu yafuatayo:-<br>Hakuna rejista ya Malalamiko ambayo imeaandaliwa au kufanyiwa maboresho na kupitiwa kwa lengo la kutambua na kuorodhesha vihatarishi vilivyotokea na pamoja na kufanya tathimini ya hatua zitakazochukuliwa kuondoa vihatarishi hivyo.<br>Hakuna mpango wa ahueni ya majanga ili kulinda mali za Halmashauri.<br>Hakuna uthibitisho wa | Menejimenti iandae Sera ya Udhibiti wa Vihatarishi na Rejista ya Vihatarishi itakayohusisha Malengo, Vihatarishi vilivyobainika/ kutambulika Kiwango cha vihatarishi, udhibiti uliofanyika, wajibu na njia za kushughulikia vihatarishi vinavyoweza kujitokeza. | Menejimenti inakubaliana na ushauri wa Mkaguzi. Kwa sasa Halmashauri imeteua Mratibu wa Usimamizi wa vihatarishi. Pia Halmashauri imewezesha watumishi 2 kuhudhuria mafunzo ya siku mbili katika Chuo Kikuu cha Mzumbe kuanzia tarehe 2-4/11/2016 yaliyohusu kujenga uelewa wa masuala ya vihatarishi.<br>Kwa sasa Mratibu amependekeza watumishi 13 mmoja kutoka kila idara watakaounda timu ya usimamizi wa vihatarishi ambao watapewa mafunzo kuhusu utambuzi, udhibiti | **Mkaguzi ameridhia Utekelezaji wa Menejimenti**<br>**Hoja imefungwa** | Hoja kama hii isijirudie tena. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kuteuliwa kwa Mratibu wa usimamizi wa vihatarishi ili kuhakikisha Sera ya Usimamizi wa Vihatarishi inatekelezwa katika ngazi zote za Tarafa. | | na njia za kukabiliana na vihatarishi hivyo. | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2.8.5** | **Ukosefu wa utoaji wa huduma endelevu Madai ya watumishi Tsh.415,054,918** Mapitio katika uongozi wa raslimali watu Manispaa ya Mpanda imebainika kuwa kumekuwepo na madai ya watumishi yasiyolipwa yenye kiasi cha Tsh.415,054,918 kama ilivyooneshwa kwenye "kiambata VII "ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu hivyo kushusha ari ya kazi jambo ambalo limeshusha utendaji wa kazi na kushusha utoaji wa huduma. Mpaka siku ya | Uongozi wa Halmashauri umeshauriwa kulipa madai yote ili kuepuka kulimbikiza madeni.<br><br>Uongozi unashauriwa kuhakikisha kuwa madai yote yanalipwa kwa wakati. | Deni linaliohusu madai ya watumishi limefanyiwa uhakiki na kuthibitishwa kuwa ni halali kwa watumishi ambao madeni hayo yalihakikiwa na kuwasilisha madeni hayo Ofisi ya Rais TAMISEMI ambapo kati ya madai yaliyopelekwa Tshs.117, 388,220 zililipwa kwa watumishi waliokuwa wanadai kupitia kwenye Mishahara yao mnamo tarehe28/2/2018.<br><br>Aidha, watumishi ambao hawakulipwa madai yao ni watumishi wale wanaokaimu nafasi za wakuu wa idara. Halmashauri imepunguza kiasi chaTsh 67,184,000.00 kati ya Tsh 321,513,305.00 kwa baadhi ya Wazabuni na jitihada za kulipa madeni hayo yaliyosalia zinaendelea. | **Halmashauri inasisitizwa kuendelea kulipa madeni** | Madeni yote yaingizwe kwenye kitabu cha hesabu za mwisho wa mwaka. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ukaguzi unafanyika mwezi Agosti, 2017 madai yalikuwa hayajalipwa. **Madeni yaliyotokana na utoaji wa huduma kiasi cha Tsh. 321,512,305.** Upimaji wa huduma zinazotolewa na Halmashauri ulibaini kuwa madeni yenye kiasi cha Tsh.415,054,918 ni madeni kutoka kwa wasambazaji wa vifaa na huduma ambayo hayajalipwa na Halmashauri. | | | | | |
| | **2.8.6.1** | **Mtandao duni unaotumika kuendesha mfumo wa malipo toleo la 9.05 (Epicor verson 9.05)** Idara ya Fedha na Uchumi ya Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda imeunganishwa kwenye mfumo wa kielektoniki wa malipo ( Epicor verson 9.05 accounting package) | Uongozi wa Halmashauri na OR-TAMISEMI ihakikishe kuwa mfumo wa kielektroniki wa malipo ( Epicor version 9.05) unahuishwa kuwezesha shughuli zote za kifedha kuendeshwa na kurahisisha mfumo wa kutoa taarifa za kihasibu na kuongeza ufanisi kwenye utoaji wa taarifa za kifedha. | Uongozi umetoa taarifa kuhusu jambo hili OR- TAMISEMI kwa barua yenye Kumb.Na KTV/MMC/S.50/4/49 ya tarehe 01/06/2017. OR-TAMISEMI inafanya kazi kuhakikisha kuwa inaboresha mfumo wa kielektroniki wa malipo (Epicor) kuenda tolea la 10 (version 10) ambao utafanya kazi kwa ufanisi zaidi. | **Maboresho ya mfumo wa epicor yafanyike na Tamisemi ili kuongeza ufanisi.** | **Menejiment iiandikie TAMISEMI barua panatakiwa maboresho.** | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Hatahivyo, Upimaji wa ufanyajikazi na ufanisi wa Epicor na mifumo mingine Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda tulibaini udhaifu kama ilivyofupishwa hapa chini:<br>Epicor IFMS inafanya kazi taratibu jambo ambalo linaathiri utoaji wa taarifa kutoka kwenye mfumo kwa wakati.<br><br>Hakuna marekebisho yoyote yanayoweza kufanywa kwa kutmia mfumo wa EPICOR kama usuluisho wa kifedha.<br><br>Kuna tatizo la mtandao kutokana na sababu mablimbali kama ukosefu wa umeme na chanzo cha umeme cha kisichoaminika. | | | | | |
| | **2.9** | **Upimaji wa viashiria vya ubadhilifu** | Uongozi wa Halmashauri inatakiwa kuweka mbinu juu ya upimaji wa udanganyifu ili kuokoa raslimali na | Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda inayo sera ya uongozi ya uthubutu ambayo inahuishwa na inapitiwa kila | **Mkaguzi ameridhia** | Hoja kama hii isijirudie | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Menejimenti ya uthubutu inapimwa mara kwa mara na inatumika kama chombo cha kufanya maamuzi kila awamu ya mradi wa jamii, ili kufanikiwa jumuia sharti iweke mpango kazi ambao utaonesha hatari na namna ya kuzidhibiti.<br><br>Upimaji wetu kwenye mazingira ya udhibiti wa ndani ya Halmashauri ya manispaa ya Mpanda tulibaini mapungufu yafuatayo:<br><br>Kutokuwepo kwa nyaraka zilizohusu menejimenti ya upimaji na udhibiti wa mfumo wa uendeshaji wa ndani unaoelezea nyenzo duni zinazozuia na kubaini udanganyifu.<br><br>Idara haikuwa na rejesta yamenejimenti ya uthubutu ambapo hatari zinazobainishwa na | kuepuka uwezekano wa upotevu wa raslimali fedha na mali nyingine. | wakati ili kupunguza hatari mbalimbali ambazo bila ukomo kwenye udanganyifu. Halmashauri ina sera inayohusu udanganyifu na si watumishi wote na madiwani wanaofahamu kuhusu udanganyifu.<br><br>Tuna mpango wa kuhakikisha kuwa watumishi na madiwani wana ufahamu na uelewa juu ya udanganyifu na masharti ya udanganyifu Halmashauri iliwaita TAKUKURU kuja kutoa elimu kwa watumishi wake wa umma ili kupata uelewa juu ya shwala hilo. | **Utekelezaji wa Menejimenti Hoja imefungwa** | tena. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | mtumishi zinaweza kuainishwa, kutathminiwa na kupunguzwa. | | | | | |
| | **2.10.1** | **Udhaifu uliobainika kwenye Mifumo ya Ukusanyaji Mapato wa Serikali za Mitaa (LGRCIS)** Mfumo ya ukusanyaji wa mapato ulizinduliwa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda kama mchakato na ulitumika kwa makusanyo ya mapato kwenye vituo vya makusanyo. Hata hivyo ili kufikia lengo la mahitaji ya jumuia na mpango kazi utakaoongoza kutambua udhaifu na jinsi ya kukabili mapungufu yafuatayo na kuutathimini mfumo. Hakuna ushahidi wa watumiaji wa mashine hizi walipata mafunzo ya namna ya kuzitumia kwa ufanisi. Kumekuwepo na kukatika kwa | Tunapendekeza Uongozi wa Halmashauri kufanya yafuatayo: Kuhakikisha kuwa mafunzo yanafanyika kuwapa uelewa watumiaji wote wa mashine za kielektroniki za mapato. Halmashauri inatakiwa kuhakikisha kuwa Mfumo wa makusanyo ya mapato uhuishwe na kuwa na taarifa zote muhimu zinazohitajika kwenye mfumo ili kufukia malengo na Halmashauri iwasiliane na Watoaji wa huduma ya mtandao kuhakikisha kuwa hakuna kukatika mara kwa mara kwa mtandao. | Kuna ushahidi kutoka kwa watumiaji wa mfumo wa kielektroniki wa malipo (POS) ambao wamepata mafunzo kuhusu namna ya kuzitumia mashine hizo. Mafunzo yaliyofanyika yaliyowahusisha wakusanya mapato wote. Uongozi utapitia na kupanga mafunzo mengine ya fedha ya mwaka 2017/2018 ili kujenga uelewa kwa watumiaji wote. | **Uhakiki wa utekelezaji wa majibu ya menejimenti utafanyika katika ukaguzi ujao.** | Menejimenti iendelee kuwajengea uwazo watumishi wa mfumo huo kuweka mafunzo kwenye bajeti yakila mwaka. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | mtandao.<br>Halmashauri ilipata changamoto ya kukiri vyanzo vingine vya fedha zilizopokelewa kutoka serikali kuu na vyanzo vingine ambapo mfumo wa kielektroniki unaowezesha mapato ya makusanyo ya ndani.<br><br>Fedha ya ruzuku iliyoletwa moja kwa moja shuleni inakluwa vigumu kuikiri kwasababu hakuna matumizi ya vitabu vya risiti.<br>Upungufu wa raslimali watu kitu kinachopunguza makusanyo ya mapato.<br>Kuna wakati mfumo hauwezi kusoma eneo mfumo wa kielektroniki wa makusanyo (POS) ulipo. | | | | | |
| | **2.10.2** | **Tofauti katika Utoaji Taarifa kati ya Mfumo wa LGRCIS na Data za Epicor** | Menejimenti ya Halmashauri ihakikishe taarifa zinazoandaliwa zinakuwa sawa ili kuwepo uwazi na uwajibikaji katika masuala ya fedha. | Halmashauri inahakiki taarifa zinazoandaliwa zinakuwa sawa ili kuweka uwazi na uwajibikaji katika masuala ya fedha.<br>Aidha, tofauti ya data iliyojitokeza | **Mkaguzi ameridhia Utekelezaji wa Menejimenti Hoja imefungwa** | Hoja kama hii isijirudie tena. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kumbukumbu za Stakabadhi za makusanyo huanzia kuwekwa katika mfumo wa LGRCIS na baadaye katika mfumo wa Epicor.<br>Ukaguzi wetu katika mfumo wa LGRCIS na katika data za Epicor ambao unahusisha ulinganisho wa kanzidata kwa mwaka wa fedha 2016/2017, tulibaini kuwa zilizomo katika mfumo wa LGRCIS ni tofauti na zile za Epicor. | Pia Menejimenti ya Halmashauri inatakiwa itoe ufafanuzi kuhusu tofauti hizo za taarifa. | katika mfumo wa LGRCIS na Epicor inatokana na namna mifumo hii inavyofanya kazi. Kwa sasa data kutoka katika mfumo wa LGRCIS zinaingizwa moja kwa moja kwenye mfumo wa Epicor wakati OR-TAMISEMI ikiendelea na jitihada za kuhakikisha mifumo hii inakuwa na utumianaji wa data wa moja kwa moja. | | | |
| | **2.10.3** | **Mapato yasiyokusanywa kutoka kwenye nyumba zilizopangishwa yenye kiasi cha TZS 64,083,900.32**<br><br>Kipindi cha mwaka ulipo kwenye mapitio, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda imekusanya kiasi cha TZS 11,676,099.68 cha mapato kutoka kwenye kodi ya nyumba tofauti na | Uongozi wa Halmashauri unatakiwa kuboresha sera ya makusanyo ya mapato yake na kuhakikisha kuwa mapato kutoka kwenye kodi ya nyumba yanakusanywa kama ilivyopangwa. | Kiasi kilichokusanywa kinaonekana kuwa ni kidogo kwa kuwa kiasi cha mapato kutoka Wizara ya Mipango na Fedha haikuwasilishwa kwa wale ambao walikuwa wamekatwa kutoka kwenye mishahara yao.<br><br>Aidha kiasi kilichowekwa kwenye bajeti kilihusisha kodi ya nyumba ambazo halmashauri ilitegemea kuzinunua zile zilizojengwa na NHC. Uongozi umechukua hatua kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kuwa wapangaji wote wasajiliwe kwenye mfumo wa LGRCIS kwenye eneo la kodi ya nyumba. Hii itawezesha makusanyo ya moja kwa moja | **Mkaguzi ameridhia Utekelezaji wa Menejimenti Hoja imefungwa** | Hoja kama hii isijirudie tena. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kile kiasi kilichopitidhwa kwenye bajeti cha TZS 75,760,000.32 ikiacha kiasi cha TZS 64,083,900.32 ambacho hakikukusanywa kwa mujibu wa ripoti ya fedha iliyowasilishwa tarehe 30.Juni, 2017. | | kutoka kwa wapangaji na kiwango stahiki kupitia tangazo/kutengeneza bili. | | | |
| | **2.10.4** | **Makusanyo ya chini kulingana na lengo la mapato kiasi cha Tsh.518,968,995.30** Halmashauri ilipanga kukusanya mapato kutoka makusanyo ya mapato ndani bila mawakala wa makusanyo ya mapato. Ili kuwa na makusanyo makubwa, Halmashauri inatakiwa kuweka malengo ambayo yatafikiwa mwisho wa mwaka. | Uongozi wa Halmashauri umeshauliwa kupitia bajeti ili kuwezesha makusanyo thabiti ya mapato. Kwa nyongeza kuwepo na ufuatiliaji thabiti na usimamizi kuhakikisha kuwa wanakusanya mapato kwa kiwango cha juu. | Halmashauri ililenga kukusanya mapato kutoka vyanzo vya mapato bila ya kuwatumia mawakala kuhakikisha kuwa malengo iliyojiwekea yamefikiwa. Mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30. Juni, 2017 ilikusanya 13% juu ya lengo lililobajetiwa kwa kutmia mashine za kielelektroni za mfumo wa ukusanyaji (POS) japo vipengele kadhaa kama kodi ya mapato, kodi ya ardhi iliyokusanywa na TRA na vipengele vingine ambavyo vilikusanywa kwa kiwango cha chini kulingana na chanzo cha makusanyo.Kwa nyongeza uongozi utaendelea kufanya ufuatiliaji. | **Mkaguzi ameridhia Utekelezaji wa Menejimenti Hoja imefungwa** | Hoja kama hii isijirudie tena. | |
| | **2.10.5.1** | **Mapungufu kwenye matumizi ya mashine ya kielektroniki ya** | Uongozi kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI umeombwa kukusanya mapungufu yote na kuhakikisha kuwa malengo ya ufungaji wa | Halmashauri kwa kushirkiana na OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa mfumo (LGRCIS) uliofungwa unaboreshwa na unafanyiwa kazi. | **Uhakiki wa utendaji wa POS utahakikiwa** | Menejimenti ihakikishe inafuatilia matumizi ya | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **ukusanyaji. (POS)** Halmashauri ya Manispa ya Mpanda imefunga mfumo wa makusanyo ya mapato na umeanza kutumika tangu Julai, 2016 kuboresha makusanyo ya mapato.<br>Tathimini ya mfumo wa kielektroniki uliowekwa Halmashauri umebaini mapungufu yafuatayo ambayo yanahitaji usimamizi na Halmashauri kuchukua hatua.<br><br>**Kutoa risiti za kukiri.**<br>Mfumo wa LGRCIS imeunganishwa kwenye mfumo wa kielektroniki wa malipo (POS).Lakini vifaa hivi viko taratibu kutoa risiti baada ya kupokea fedha kutoka kwa walipa kodi.<br><br>Kuna tatizo la mtandao mara chache kutokana na sababu kama | mfumo (LGRCIS) yanafikiwa. | Mapungufu yaliyobainishwa yanaboreshwa na matatizo husika ya kila siku yanatolewa taarifa OR-TAMISEMI kwa marekebisho.<br><br>Mtunza Hazina tayari amewekwa kwenye mfumo wa kuthibiutisha marekebisho ya bili kama itahitajika. Vifaa vilinunuliwa kwa kuwa na hati ya mwaka mmoja.<br><br>Stakabadhi ya POS kwa ajili ya uthibitisho wa ukaguzi ipo.<br><br>Ripoti ya kiufundi ya vifaa ya manunuzi ya agizo 58(2) ya LGFM, 2009 ni LGA.101/2016/17/CQ/G/03.<br>Cheti kilichosainiwa cha matengenezo na majaribio yako tayari kwa wadau na zimeambatishwa kwenye hati ya malipo ya malipo. | **katika ukaguzi ujao** | POS kwa ukaribu, watumiaji wa POS waendelee kujengewa uwezo. | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kutokuwepo umeme, kuchelewa kuwekewa vifurushi vya mtandao kwenye POS.<br>POS haitumiki kurekodi makusanyo ya mapato (POS-nje ya mtandao)<br>Hakuna waranti iliyotolewa kwenye vifaa vya kielektroniki vilivyonunuliwa/Hakuna mkataba wa huduma.<br>Hakuna namba za utambulisho ya maalum (namba mficho) zilizotolewa kuzitofautisha na vifaa vingine vya kielektroniki<br>Hakuna stakabadhi ya POS kwa ajili ya uthibitisho wa ukaguzi.<br>Hakuna ripoti ya kiufundi ya vifaa vilivyonunuliwa kwa kanuni 58(2) ya LGFM, 2009 unaosisitiza kuwa vifaa na huduma ni vya kiufundi, Mafundi walitakiwa kushirikishwa kabla ya kuvikubali vifaa au | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | huduma.<br>Cheti cha ukaguzi na majaribio kilichosainiwa kipelekwe kwa wadau na au kiambatishwe kwenye hati ya malipo ya malipo.<br>Vifaa vya kielektroniki vya makusanyo ya mapato (POS) vilibainika kukwama kwenye mfumo na havikuweza kusafirisha taarifa za mapato ya makusanyo kutoka kwenye kanzi data ya LGRCIS toleo sabili (Point of Sale Version-POS) imekuwa na changamoto ya kuunganisha msimbo wa masahahisho ya makusanyo kwa kutokuwepo taarifa sahihi za makusanyo ya mapato na kuripoti.<br>Watu muhimu kama Mtunza Hazinahawajawekwa kwenye mfumo hivyo kuidhinisha na kukubali kupitia kwenye mfumo | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | inakuwa vigumu. | | | | | |
